(2) Notwithstanding the repeal of the Apprentices Decree by subsection (1) of this section every contract of apprenticeship existing immediately before the commencement of this Act shall continue in force and be reduced to writing and executed and registered in accordance with the procedure laid down in section 13 of this Act within four months of the date of commencement of this Act.

Passed in the House of Representatives
on the 16th day of December, 1986.



SALIM MZEE

ACTING CLERK OF THE HOUSE
OF REPRESENTATIVES.

SHERIA YA KUFUTA NA KUENZISHA UPYA
SHERIA YA WANAFUNZI WA KAZI (APPRENTICES) NA
KUWEKA MASHARTI BORA ZAIDI KUHUSIANA NA
MAFUNZO KWA WANAFUNZI WA
KAZI WATU WENGINE VIWANDANI.

KIFUNGU:

SEHEMU YA KWANZA

1. Jina na tarehe ya kuanza kutumika.
2. Matumizi ya Sheria.
3. Ufafamuzi.

SEHEMU YA PILI

4. Uteuzi wa Mkurugenzi na Msaidizi wa Mafunzo ya Amali.
5. Kazi za Mkurugenzi.
6. Uanzishwaji wa Baraza la Taifa la Mafunzo na Wajumbe wote.
7. Mikutano ya Baraza.
8. Kazi za Baraza.
9. Kamati ya Mafunzo.

SEHEMU YA TATU.

10. Ruhusa ya kuajiri wanafunzi wa kazi na wanafunzi wanaobanwa na mikataba.
11. Mtu anayeweza kujifunga (bind) kama ni mwanafunzi wa kazi au mwanafunzi anayebanwa na Mikataba.
12. Uangalizi wa afya kwa wanafunzi wa kazi.
13. Kumbukumbu ya mikataba ya wanafunzi wa kazi.
14. Uhamisho wa Mikataba ya wanafunzi wa kazi.
15. Kuvunjwa kwa mikataba.
16. Kumshawishi mwanafunzi wa kazi au mwanafunzi aliyetilishwa mkataba.
17. Kipindi cha majaribio.
18. Mwanafunzi wa kazi aliyebanwa na mkataba kupata mshahara baada ya kumaliza mkataba.
19. Kusimamishwa mwanafunzi wa kazi au yule aliyetilishwa mkataba.
20. Waajiri kuweka kumbukumbu.
21. Mipaka kuhusu utaratibu wa malipo.

KIFUNGU:

22. Stashahada ya kumaliza muda wa uanafunzi.

SEHEMU YA NNE

23. Mkurugenzi anaweza kufanya mapendekezo ya mipango ya mafunzo.
24. Uwezo wa Waziri kufanya mpango wa mafunzo.
25. Usimamiwaji wa mwanafunzi wa mfanyakazi wa mkataba.

SEHEMU YA TANO.

26. Uwezo wa Mkurugenzi.
27. Uteuzi wa Wakaguzi.
28. Uwezo wa Mkaguzi.

SEHEMU YA SITA

29. Kutoa maelezo ni kosa.
30. Kamuni.
31. Kufungua mashtaka.
32. Adabu.
33. Kufutwa kwa Cap. 57

SHERIA NAMBA 17.....

NAKUBALI

Idris Abdul Sahil

IDRIS ABDULWAKIL

RAIS WA ZANZIBAR

NA MWENYEKITI WA

BARAZA LA MAPINDUZI.

9 Februari 1987.

SHERIA YA KUFUTA NA KUENZISHA UPYA
SHERIA YA WANAFUNZI WA KAZI (APPRENTICES) NA
KUWEKA MASHARTI BORA ZAIDI KUHUJIANA NA
MAFUNZO KWA WANAFUNZI WA
KAZI NA WATU WENGINE VIWANDANI.

IMEITUNGWA na Baraza la Wawakilishi la Zanzibar.

SEHEMU YA KWANZA

Jina na
tarehe ya
kuanza
kutumika.

1. Sheria hii itajulikana kuwa ni Sheria ya Mafunzo ya
Amali (Vocational Training) 1986 na itaanza kutumika tarehe
ambayo Waziri ataitangaza katika Gazeti Rasmi la Serikali.

Matumizi ya
sheria hii.

2. (1) Pamoja na masharti yaliyomo kwenye kijifungu cha (2)
cha kifungu hiki, Sheria hii haitowahusu wafuatao:-

- (a) Askari wa Jeshi la Ulinzi la Jamhuri ya
Muungano;
- (b) Askari wa Jeshi la Polisi;
- (c) Askari wa Idara Maalum za Serikali ya
Mapinduzi ya Zanzibar.

Kusameheka
na masharti ya
sheria hii.

(2) Waziri kwa kutoa Tangazo kwenye Gazeti anaweza
kukisamehe Chombo au Vyombo vyovyote vya Serikali
au mtu ye yote au kikundi fulani cha watu kutokana
na vifungu au baadhi ya vifungu vya sheria hii au
kutokana na kamuni au amri iliyotolewa chini ya
Sheria hii au kutokana na masharti ye yote ya
uanafunzi wa kazi au mkataba wa kujifunza uliomo
kwenye mpango wa mafunzo (scheme) yoyote.

Ufafanuzi

3. Katika sheria hii, isipokuwa kama itaelezwa vyenginevyo:-

"Mwanafunzi wa kazi (apprentice)" maana yake ni mtu anaefungwa kwa mkataba kufanya kazi chini ya muajiri kwa kipindi fulani kisichopungua miaka mime au chini ya muda huo kama itakavyoamuliwa na Baraza kufuatana na maelezo kwenye kifungu cha 26(2) cha sheria hii kwa madhumuni ya kupata elimu ya biashara ambayo muajiri atalazimika kumfundisha mwanafunzi huyo,

"Kamati" maana yake ni Kamati ya mafunzo iliyoanzishwa chini ya kifungu cha 9 cha Sheria hii;

"Baraza" maana yake ni Baraza la Taifa la Mafunzo ya Amali lililoanzishwa chini ya kifungu cha 6 cha Sheria hii;

"Mkurugenzi" maana yake ni Mkurugenzi wa Mafunzo ya Amali aliyeteuliwa chini ya kifungu cha 4 cha Sheria hii;

"Mwanafunzi aliyetilishwa mkataba (indentured learner)" maana yake ni mtu ambaye si mwanafunzi wa Kazi, ambaye anabanwa (bound) na mkataba amtumikie muajiri wake kwa kipindi kisichozi miaka mime kwa nia ya kupata ujuzi ambao muajiri atawajibika amfunze;

"Mkaguzi" maana yake ni mkaguzi aliyeteuliwa na Waziri chini ya kifungu cha 27 cha Sheria hii na inajumuisha Mkurugenzi;

"Ujuzi" ni pamoja na nadharia na vitendo katika kazi;

"Ofisa wa kazi" maana yake ni mtu aliyeteuliwa kufanya kazi za Serikali kama ni Mkurugenzi wa Kazi, Msaidizi Mkurugenzi wa Kazi, Ofisa wa Kazi Mwandamizi (Principal Labour Officer), Ofisa Mkuu wa Kazi au Ofisa wa Kazi;

"Waziri" maana yake ni Waziri anaohusika na mambo ya kazi;

"Mtoto" maana yake ni mtu mwenye umri usiotimia miaka kumi na tano;

"M. pango" maana yake ni mpango ulioainishwa kwenye kifungu cha 24 wa kuongoza mafunzo ya wanafunzi wa kazi au wanafunzi waliotilishwa mikataba katika kazi yoyote;

"Idara Maalum" maana yake ni Idara Maalum zilizoanzishwa chini ya kifungu cha 120 cha Katiba ya Zanzibar ya mwaka 1984;

"Kazi" maana yake ni kazi inayohitaji ujuzi (skill).¹

SEHEMU YA PILI

UANZISHWAJI NA UTAWALA WA BARAZA
LA TAIFA LA MAFUNZO YA AMALI.

Uteuzi wa
Mkurugenzi na
Msaidizi
Mkurugenzi wa
Mafunzo ya
Amali.¹

4. (1) Waziri atamteua mfanyakazi wa Serikali mwenye uwezo na sifa zinazokubalika kuwa Mkurugenzi na kuteua idadi ya wanafunzi wengine wa Serikali wenye sifa zinazokubalika kuwa wasaidizi Wakurugenzi wa Mafunzo ya Amali kwa mujibu wa Maelezo ya Sheria hii.¹

(2) Kila Msaidizi Mkurugenzi wa Mafunzo ya Amali, baada ya kufuata muongozo wa Mkurugenzi, atafanya kitendo chochote au kazi yoyote ambayo kisheria inaweza kufanywa na Mkurugenzi kwa mujibu wa maelezo ya sheria hii.¹

Kazi za
Mkurugenzi.¹

5. Mkurugenzi atawajibika kufanya kazi zifuatazo:-

- (a) Kuhakikisha muongozo na mafunzo yanaelekezwa kwenye kutambua na kuendeleza vipawa vya binadamu kwa ajili ya usalishaji na utoshelezaji wa mahitaji mahitaji ya mfanyakazi na kwa madhumuni ya kuinua kiwango chake cha elimu ili kupata ufanisi zaidi kazini;

- (b) Kuhakikisha kuwepo kwa sera na utaratibu kamili wa usimamizi wa mafunzo ya kazi utakao ainishwa na uajiri pamoja na kubuni nafasi za kazi (creation of employment);
- (c) Kuhakikisha kwamba mafunzo ya amali yanakidhi haja kwa wanafunzi wote na yanalenga katika kupata usawa baina ya wananchi wa Mijini na Mashamba;
- (d) Kutenda kazi nyengine zihusuzo wanafunzi wa mafunzo ya amali na wale waliofungwa na mikataba kwa mujibu wa maelezo ya sheria hii.

Uanzishwaji wa
Baraza la
Taifa la
Mafunzo ya Amali
na Wajumbe wote.

6. (1) Panaanzishwa Baraza litakalojulikana kuwa ni Baraza la Taifa la Mafunzo ya Amali.

(2) Baraza litakuwa na Mwenyekiti ataeteuliwa na Rais, pamoja na Wajumbe wafuatao ambao watateuliwa na Waziri:-

- (a) Mkurugenzi wa Idara ya kazi
- (b) Muwakilishi mmoja kutoka Tume ya Mipango
- (c) Muwakilishi kutoka Utumishi kutoka Serikalini
- (d) Mjumbe mmoja kutoka elimu ya juu
- (e) Mjumbe mmoja kutoka Juwata
- (f) Mjumbe mmoja kutoka Baraza la Wawakilishi
- (g) Mmoja kutoka Mbunge wa Muungano
- (h) Mmoja kutoka Jumuiya ya Waajiri
- (i) Wajumbe wanne ambao ni mafundi Zanzibar ambao watateuliwa na Waziri.

(3) Msaidizi Mwenyekiti atateuliwa na Wajumbe wa Baraza kutoka na miongoni mwao.

(4) Mkurugenzi au Mwakilishi wake atakuwa ni Katibu wa Baraza ambaye ndiye atakaewajibika kuweka kumbukumbu za mikutano na shughuli zote za Baraza.

(5) Mwenyekiti na Wajumbe watahika nyadhifa zao kwa kipindi cha miaka mitatu na wanaweza kuteuliwa tena kwa kipindi chengine.

Mikutano ya
Baraza.

7. (1) Kufuatana na masharti ya Kamuni zitakazotungwa ohini ya Sheria hii na kufuatana na miongozo ya Mkurugenzi, Baraza litakutana angalau mara moja katika kila miezi miwili.

(2) Mikutano wowote wa Baraza utafanyika iwapo zaidi ya nusu ya Wajumbe wote wamehudhuria.

Kazi za
Baraza.

8. Pamoja na masharti ya sheria hii, Baraza litawajibika kufanya kazi zifuatazo:-

- (a) Kupanga mafunzo maalum ya amali yatakayokwenda sambamba na kazi za uzalishaji kwa vijana wasiokuwa na kazi;
- (b) Kupanga utaratibu wa kuinua viwango vya elimu na ufundi kwa vijana wadogo na watu wazima waliomo makazini kwa madhumuni ya kuongeza ujuzi wao katika utendaji kazi na kuwapa nafasi zaidi za kujiendeleza;
- (c) Kuwapa misingi ya uelekeo na hamu ya kazi vijana na watu ambao bado hawajaajiriwa kwa nia ya kuwapa nafasi ya kuchaguwa aina ya elimu au mafunzo ya amali kulingana na uwezo na hamu zao;
- (d) Kuhakikisha kwamba mafunzo ya kazi yanalenga katika kazi za uzalishaji ikiwa ni pamoja na kazi za binafsi kwa nia ya kuamsha na kuendeleza ugunduzi (creativity) katika kupata ufanisi kazini pamoja na kuwalinda watu dhidi ya ukosefu wa kazi unaotokana na kutokuwepo haja ya wafanyakazi wa fani hiyo au kwamba wafanyakazi wa fani hiyo wamekuwa wengi kupita kiasi;
- (e) Baraza linaweza au baada ya kuombwa na Mkurugenzi kufanya uchunguzi na kutoa mapendekezo yake kwa Mkurugenzi kuhusiana na suala lolote ohini ya sheria hii;

- (f) litachunguza mzozo au jambo lolote litakalozuka kutokana na mkataba wa mwanafunzi wa kazi au mwanafunzi anayebanwa na mkataba huo baada ya kuletewa mzozo huo na Mkurugenzi na Baraza litawajibika kutatua mzozo huo kihaki;
- (g) lifafanya kazi nyengine kuhusiana na wanafunzi wa kazi na wanafunzi waliobanwa na mkataba kama itavyojiri;
- (h) litahakikisha kupatikana kwa wafanyakazi waliofunzwa vizuri katika viwango vyote kila wanapohitajika;
- (i) litahakikisha kupatikana kwa viwango vya juu kabisa na ufanisi katika mafunzo ya Amali.

Kamati ya
Mafunzo.

9. (1) Baraza linaweza kuanzisha Kamati za Mafunzo zifuatazo kwa madhumuni ya kufanya kazi za Baraza kuhusiana na mafunzo:-

- (a) Mafunzo na Uchambuzi wa ustadi;
- (b) Majaribio ya kazi;
- (c) Utafiti, Ugunduzi na Maendeleo;
- (d) Mipango na Fedha.

(2) Mbali na yale yaliyoelezwa kwenye kijifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki Baraza linaweza kuunda Kamati nyengine yeyote kuhusiana na mafunzo au shughuli nyengine za Baraza.

(3) Wajumbe wa Kamati za Mafunzo au Wajumbe wa Kamati nyengine zilizoundwa ohini ya kifungu hiki watateuliwa toka miongoni mwa Wajumbe wa Baraza au nje yake au sehemu zote mbili:
Isipokuwa jumla ya Wajumbe hao haitozidi watano angalau Mjumbe mmoja awe Mwakilishi toka Muungano wa Waajiri na mmoja toka JUWATA.

(4) Mwenyekiti na Wajumbe wengine wa Kamati watahika nyadhifa zao kwa kipindi kisichozidi kipindi cha Wajumbe wa Baraza na wanaweza kuteuliwa tena kwa kipindi chengine.

(5) Kulingana na masharti ya miongozo ama ya jumla au maalum itakayotolewa na Baraza, na kwa mujibu wa masharti ya sheria hii au kanuni zozote zitakazotungwa chini ya sheria hii, Kamati itapanga utaratibu wake wenyewe wa kuendesha shughuli zake.

(6) Mkurugenzi au Mwakilishi wake atakuwa ni Katibu wa Kamati yeyote itakayoundwa chini ya kifungu hiki.

(7) Kamati itafanya shughuli zake kwa niaba ya Baraza kama itakavyopewa uwezo wa aina hiyo na Baraza lenyewe kwa maandishi, na itafanya shughuli hizo kwa kushauriana na Mkurugenzi.

SEHEMU YA TATU.

MAELEZO KUHUSU MIKATABA YA WANAFUNZI

WA KAZI NA WANAFUNZI WANAObANWA NA

MIKATABA.

Ruhusa ya
kuajiri
wanafunzi
wa kazi na
wanafunzi
wanaobanwa
na mikataba.

10. (1) (a) Hakuna mtu atakae mwajiri mwanafunzi wa kazi au mwanafunzi aliyebanwa na mikataba kabla hajaruhusiwa kimaandishi na Mkurugenzi kufanya hivyo.

(b) Ruhusa ya Mkurugenzi itaainisha idadi ya jum kabisa ya wanafunzi ambao wanaweza kuajiri kwa wakati mmoja na mtu huyo aliyepewa ruhusa hiyo.

(2) Hakuna ruhusa itakayotolewa chini ya kifungu hiki isipokuwa muombaji amtoshe Mkurugenzi kwamba kazi yake itatoa nafasi nzuri ya mafunzo kwa idadi ya wanafunzi wanaopendekeza kuwaajiri.

(3) Mtu ye yote ambaye hakuridhika na uamuzi wa Mkurugenzi chini ya kifungu hiki anaweza kukata rufaa kwa Waziri ambaye uamuzi wake utakuwa ni wa mwisho.

(4) Mtu ye yote ambaye :-

- (a) amejiri mwanafunzi wa kazi au mwanafunzi aliyebanwa na mkataba kabla ya kupata ruhusa ya maandishi toka kwa Mkurugenzi; au
- (b) baada ya kupata ruhusa ya kuajiri idadi fulani ya wanafunzi wa kazi au wanafunzi wanaobanwa na mkataba, akaajiri zaidi ya idadi ile aliyoruhusiwa kwa maandishi, atakuwa ni mkosa.

Mtu anayeweza kujifunga (bind) kama ni mwanafunzi wa kazi au mwanafunzi anayebanwa na Mkataba.

11. (1) Mtu ye yote ambaye-

- (a) ametimia umri wa miaka kumi na tano;
- (b) amemaliza elimu ya lazima kwa mujibu wa sheria
- (c) kuhusiana na kazi ambayo mpango umewekwa, anazo sifa kwa mujibu wa mpango huo; na
- (d) amethibitishwa kuwa afya yake vizuri kwa mujibu wa kifungu cha 12 anaweza kufuatana na masharti ya kifungu kidogo cha (3) cha kifungu hiki akajifunga mwenyewe kama ni mwanafunzi wa kazi au mwanafunzi anayebanwa na mkataba katika shughuli yoyote.

(2) Hakuna mtu ambaye hana sifa zilizoelezwa chini ya kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki atakayejifunga mwenyewe kama mwanafunzi wa kazi au aliyebanwa na mkataba.

(3) Mtu ambaye ni mtoto mdogo hatojifunga kuwa mwanafunzi wa kazi au mwanafunzi anayebanwa na mkataba isipokuwa kwa idhini ya wazazi wake na iwapo hana wazazi wala walezi bali lazima ipatikane idhini ya afisa wa kazi.

(4) Mtoto ambaye, baadaya kupata idhini kwa mujibu wa maelezo ya kifungu kidogo cha (3) cha kifungu hiki, amejifunga mwenyewe kama mwanafunzi wa kazi au aliyebanzwa na mkataba, basi atabarwa na mkataba huo kwa wakati wote hata kama katika kipindi hicho atakuwa mtu mzima.

Uangalizi wa afya kwa wanafunzi wa kazi.

12. Kila mtu kabla ya kuingia katika mkataba wa Uanafunzi wa kazi itabidi aangaliwe afya yake na daktari ambaye baadaye atatoa cheti kuthibitisha kwamba mtu huyo anafaa/hafai kuaajiriwa kwa kazi inayohusika.

Kumbukumbu ya mikataba ya wanafunzi wa kazi.

13. (1) Kila mkataba wa kazi au mkataba unaombana mwanafunzi wa kazi ulioingiwa baada ya kuanza kutumika kwa sheria hii, utakuwa katika umbile maalum litakalowekwa na iwapo hakuna umbile hilo basi utakuwa na umbo litakalokubaliwa na Mkurugenzi.

(2) Muajiri anayeingia kwenye mkataba wa uanafunzi wa kazi na mtu ye yote atalazimika, katika kipindi kisichozidi siku kumi na nne, kupeleka kwa Mkurugenzi ili kuandikisha -

- (a) Mkataba wa uanafunzi wa kazi au wa mtu anayebanwa na mkataba wa mujifunza;
- (b) nakla ya mkataba huo;
- (c) nakla nyengine zaidi ili itive kwenye jalada la Mkurugenzi;
- (d) karatasi ya hospitali iliyopatikana kwa mujibu wa kifungu cha 12.

(3) Muajiri yoyote atakaekwenda kinyume na maelezo ya kifungu kidogo cha (2) cha kifungu hiki atakuwa na makosa.

(4) Hakuna mkataba wa uanafunzi wa kazi ulioingiwa baada ya kuanza kutumika sheria hii utakaokuwa na nguvu za Kisheria isipokuwa uandikishwe (registered) na Mkurugenzi.

(5) Mkurugenzi anaweza kukataa kuandikisha mkataba wowote wa uanafunzi wa kazi iwapo ataona kuwa hauna maslahi kwa mwanafunzi wa kazi au yule aliyetilishwa mkataba huo, au iwapo

mkataba huo haukufanywa kwa mujibu wa mpango; na katika kufikia uamuzi huo anaweza, mbali na sababu nyengine yoyote, kutilia maanani uwezekano wa mwanafunzi huyo kupata nafasi ya kazi baada ya kumalizika mkataba huo katika kazi ambayo anakusudia mkataba huo umfunge.

(6) Mtu yeyote ambaye hakuridhika na uamuzi wa Mkurugenzi kukataa kuandikisha mkataba huo anaweza kukata rufaa kwa Waziri katika muda usiozidi siku thalathini tokea siku Mkurugenzi alipotoa uamuzi wake, na uamuzi wa Waziri utakuwa ni wa mwisho.

(7) Katika kila kesi ambapo Mkurugenzi ameuandikisha mkataba chini ya Sheria hii, atafanya yafuatayo -

- (a) atatia masuala yote ya uandikishaji kwenye mkataba huo na nakla yake kama ulivyoolezwa kwenye aya ya (b) ya kijifungu kidogo cha (2) cha kifungu hiki, na kuurudisha mkataba huo na nakala yake kwa muajiri; na
- (b) atatia kwenye jalada nakla iliyoelezwa kwenye aya ya (c) ya kijifungu kidogo cha (2) cha kifungu hiki.

(8) Muajiri atatoa nakla moja ya mkatana iliyo-thibitishwa (endorsed) kwa mujibu wa kijifungu kidogo cha (7) cha kifungu hiki na kumpa mwanafunzi wa kazi au mwanafunzi aliyebanwa na mkataba wa kazi.

Uhamisho
wa Mikataba
ya uanafunzi
wa kazi.

14. (1) Haki na majukumu ya muajiri chini ya mkataba wowote wa uanafunzi wa kazi zinaweza kuhamishiwa kwa muajiri mwengine kwa makubaliano na mwanafunzi mwenyewe na baada ya kuidhinishwa na Mkurugenzi.

(2) Mkurugenzi anaweza kukataa kuidhinisha uhamisho huo iwapo ataona hautakuwa na maslahi kwa mwanafunzi wa kazi au mwanafunzi aliyetilishwa na mkataba huo.

(3) Kwa kufuatana na masharti yaliopo kwenye kijifungu kidogo cha (5) cha kifungu hiki, hakuna uhamisho wahaki na majukumu ya muajiri utakaokuwa umetimia mpaka nyaraka za uhamisho -

- (a) ziwekwe katika maandishi na zitiwe sahihi na/au kwa niaba ya muajiri anayetoa uhamisho huo pamoja na sahihi ya mwanafunzi wa kazi au mwanafunzi aliyetilishwa mkataba; na iwapo mwanafunzi huyo wa kazi ni mtoto mdogo, basi pale nyaraka hizo zinapotiwa sahihi na wazazi au mlezi na kama hana wazazi wale mlezi, pale nyaraka hizo zinapotiwa sahihi na ofisa wa kazi; na
- (b) mpaka nyaraka hizo zilandikishwe na Mkurugenzi kwa mujibu wa maelezo ya kijifungu kidogo cha (4) cha kifungu hiki.

(4) Yule muajiri ambaye haki na majukumu chini ya mkataba wa uanafunzi wa kazi yanapelekwa kwake atalazimika, katika kipindi kisichozidi mwezi mmoja tokea atie sahihi nyaraka hizo za uhamisho, apeleke nyaraka hizo kwa Mkurugenzi ili zilandikishwe. Muajiri ye yote atakaewacha kupeleka nyaraka hizo kuandikishwa basi atakuwa na makosa.

(5) (a) Pale mwanafunzi wa kazi au mwanafunzi aliyetilishwa mkataba anapojiriwa na watu wawili au zaidi katika usia (partnership), isipokuwa kama ataamua mwenyewe, mkataba wake hautamalizika kwa kifo au kustaafu kwa mtu mmoja au zaidi kwenye usia huo iwapo bado usia wenyewe umaendelea, na haki na majukumu chini ya mkataba huo zitahesabiwa kwenda kwa wale watu (partners) wanaoendelea na usia huo.

- (b) Yule mtu au watu ambao wanaendelea na usia huo watalazimika, katika kipindi kisichozidi mwezi mmoja tokea kufa riki au kustaafu huko, kupeleka mkataba huo kwa Mkurugenzi kama kwamba mwanafunzi wa kazi anataka kuhamishwa (transferred) na Mkurugenzi atathibitisha kwa kuweka sahihi kwamba haki na majukumu yote ya muajiri yanawekwa kwa wanachama wa usia huo waliobaki.

Kuvunjwa
kwa
mikataba.

15. (1) Bila ya kuathiri maelezo ya kifungu cha 21 cha Sheria hii, kila mkataba wa uanafunzi wa kazi anaweza kuvunjwa -

- (a) kwa makubaliano yapande zote, na iwapo mwanafunzi wa kazi au wanafunzi anayebanwa na mkataba huo ni mtoto mdogo basi lazima ipatikane idhini kamili inayotakiwa kabla ya mtoto huyo haijaingia kwenye mkataba wa kazi; au
- (b) na Mkurugenzi kutokana na matakwa ya upande wowote na iwapo ataridhika kwamba ni vyema auvunje mkataba huo; na
- (c) na Mkurugenzi baada ya kutakiwa kufanya hivyo na Baraza.

(2) Muajiri atatoa notisi kwa Mkurugenzi kuhusu kuvunjwa kwa mkataba wowote chini ya aya ya (a) ya kijifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki, na muajiri yoyote atakaeshindwa kutoa notisi ya namna hiyo katika kipindi cha mwezi mmoja atakuwa na makosa.

(3) Mkurugenzi hatotumia uwezo wake aliopewa chini ya aya (b) ya kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki mpaka kwanza azipe pande zote mbili kwenye mkataba huo nafasi za kujieleza ama kwa mdomo au maandishi.

(4) Mkurugenzi atasaini katika nakla ya mkataba wa uanafunzi wa kazi ulioandikishwa kwamba mkataba huo sasa umevunjwa.

(5) (a) Pale mkataba wa uanafunzi wa kazi unapovunjwa na Mkurugenzi chini ya kifungu hiki, Mkurugenzi anaweza, baada ya kushauriana na Baraza, kutoa muongozi kuhusu ulipaji wa mishahara yoyote kwa wanafunzi wa kazi au wale wanapbanwa na mikataba ya kazi ambayo kama si kuvunjwa kwa mkataba huo ingebidi walipwe.

(b) Mtu ye yote ambae hakuridhika na kitendo cha Mkurugenzi kuvunja mkataba wa wanafunzi wa kazi au kuhusu kuugawanya mishahara yao anaweza kukata rufaa kwa Waziri katika kipindi kisichozidi miezi miwili tokea aupate uamuzi wa Mkurugenzi.

(6) Uamuzi wa Waziri chini ya aya (b) ya kifungu kidogo cha (5) cha kifungu hiki utakuwa ni wa mwisho na utathibitishwa na Mkurugenzi katika nakala ya mkataba wa uanafunzi ulioandikishwa.

(7) Mkataba utakaovunjwa chini ya kifungu hiki utahesabiwa hivyo kwa madhumuni yote lakini hiyo haitaathiri madai ya haki yaliokuwepo kabla ya tarehe ya kuvunjwa kwa mkataba huo.

16. Mtu ye yote atakaemshawishi au atakaejaribu kumshawishi mwanafunzi wa kazi au mwanafunzi aliyetilishwa mkataba kukimbia kazi toka kwa muajiri wake, au ambae amemwajiri mtu akijuwa kuwa mtu huyo ni mwanafunzi wa kazi au amebanwa na mkataba, atakuwa na makosa na likithibiti atatozwa faini isiyozidi shilingi elfu mbili.

17. (1) Bila ya kuathiri maelezo ya kifungu cha 19 cha sheria hii, kipindi cha miezi sita ya mwanzo ya kila mkataba wa mwanafunzi wa kazi kitahesabiwa kuwa ni cha majaribio ambapo katika kipindi hicho upande wowote unaweza kuamua kuvunja mkataba huo; na makubaliano yoyote yatakayokuwa kinyume na maelezo hayo yatakuwa hayafai hata kama yatakuwa ni sehemu ya mkataba wa kazi.

(2) Muajiri atatoa notisi kwa Mkurugenzi kuhusu kuvunjwa kwa mkataba wowote chini ya kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki, na muajiri yeyote atakaewacha kufanya hivyo katika kipindi cha mwezi tokea kuvunjika mkataba huo basi atakuwa ni mkosa.

18. Iwapo mtu ye yote ambaye amepewa dhamana ya mwanafunzi wa kazi au anaebanwa na mkataba akaendelea kufaidika na huduma zao bila ya kuwepo makubaliano yoyote basi mwanafunzi hao watastahiki kupata kutoka kwa mtu huyo mishahara ambayo wafanyakazi wanaotoa huduma kama hiyo wanapata.

Kumshawishi
mwanafunzi
wa kazi au
mwanafunzi
aliyetilishwa.

Mwanafunzi wa
kazi aliyebanwa
na mkataba kupata
mishahara baada
ya kumaliza
mkataba.

Kusimamishwa
mwanafunzi
wa kazi au
yule aliye-
tilishwa
mkataba.

19.(1) Iwapo muajiri ametoshaka kwamba mwanafunzi wa kazi au aliyetilishwa mkataba chini ya sheria hii amefanya kitendo kikubwa cha kuvunja masharti ya mkatabahuo au masharti yoyote ya uanafunzi wa kazi yamuhusuyo mwanafunzi huyo, anaweza kumsimamisha (suspend) kazi mwanafunzi huyo.

(2) Muajiri anaemsimamisha mwanafunzi wa kazi au yule aliyetilishwa mkataba atalazimika kutoa ripoti, katika muda usiozidi siku tatu, kwa mkaguzi ambaye nae atapeleka nakla ya ripoti hiyo kwa Mkurugenzi. Baadaye Mkurugenzi atachunguza au ataamuru kuchunguzwa shauri hilo na baada ya kwisha uchunguzi huo atathibitisha au atafuta usimamishwaji huo au atabadilisha masharti ya mkataba.

(3) Iwapo malalamiko ya muajiri yamepelekwa au la, Mkurugenzi anaweza kuamuru kusimamishwa mwanafunzi wa kazi au yule aliyetilishwa mkataba, wakisubiri uchunguzi umalizike, na iwapo atafanya hivyo atawajibika aripoti kwa Baraza.

(4) Pale Mkurugenzi anapofuta amri ya kumsimamisha mwanafunzi wa kazi au aliyetilishwa mkataba, muajiri atawajibika kumlipa mwanafunzi huyo mishahara yake yote aliyoikosa wakati alipokuwa amesimamishwa.

(5) Muajiri yeyote ataewacha kuripoti kusimamishwa kwa mwanafunzi wa kazi au aliyebarwa na mkataba kama ilivyo-elezwa kwenye kifungu hiki atakuwa ni mkosa.

Wajajiri
kuweka
kumbukumbu.

20.(1) Kila muajiri alieajiri mwanafunzi wa kazi au aliyetilishwa mkataba atawajibika kuweka kumbukumbu ya kila mwanafunzi kuhusu malipo, masaa ya kazi pamoja na mambo mengine kama itakavyoelezwa na kwamba kumbukumbu hizo zitawekwa katika mfumo na utaratibu utakaoamriwa.

(2) Kila mtu anaeajiri au alieajiri mwanafunzi wa kazi au aliyetilishwa mkataba atahifadhi kumbukumbu zilizowekwa kwa mujibu wa maelezo ya kifungu hiki kwa kipindi cha miaka mitatu tokea tarehe ya mwisho ya kuandika kitu (last entry) kwenye kumbukumbu hizo.

(3) Kila muajiri atakaeshindwa kuweka kumbukumbu nzuri katika mfumo na utaratibu unaotakiwa, na kila muajiri au aliyekuwa muajiri atakaeshindwa kuweka kumbukumbu kwa kipindi kinachotakiwa kwa mujibu wa maelezo ya kifungu hiki atakuwa na makosa.

Mipaka kuhusu utaratibu wa malipo.

21. Bila ya kuathiri maelezo ya Sheria nyengine yeyote inayotumika, masharti yoyote ya mkataba wa mwanafunzi wa kazi au yule aliyetilishwa mkataba ambayo -

- (a) yanaeleza kwamba mshahara wote au sehemu yake utalipwa kulingana na kiwango cha kazi atakachofanya; au
- (b) yanayomtaka mwanafunzi wa kazi au yule aliyetilishwa mkataba ambaye umri wake ni chini ya miaka kumi na saba kufanya kazi baada ya saa za kazi (Overtime)

Stashahada ya kumaliza muda wa uanafunzi.

22.(1) Muajiri wa kila mwanafunzi wa kazi au mwanafunzi aliyetilishwa mkataba baada ya kuombwa na mwanafunzi, atalazimika, iwapo mwanafunzi huyo amemaliza vizuri mkataba wake wa uanafunzi ampe mwanafunzi huyo stashahada itakayokuwa na umbile maalum Muajiri ataipeleka stashahada hiyo kwa Mkurugenzi ambaye atatia sahihi yake na muajiri atampa mwanafunzi huyo aliyehitimu.

(2) Iwapo muajiri ye yote ameshindwa kutoa stashahada ya aina hiyo, basi bila ya kuathiri adhabu nyengine ye yote anayoweza kutiwa, itakuwa ni halali kwa Mkurugenzi baada ya kuulizia mambo hayo, kutoa stashahada hiyo yeye mwenyewe.

(3) Mtu ye yote atakaekwenda kinyume na maelezo ya kijifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki atakuwa na makosa.

(4) Mtu ye yote atakaempa stashahada ya uwongo mwanafunzi wa kazi au yule anaebanwa na mkataba akijuwa kwamba stashahada hiyo ni ya uwongo atakuwa na makosa.

SEHEMU YA NNE

MPANGO WA MAFUNZO.

23.(1) Pamoja na masharti yaliyomo katika kifungu hiki, Mkurugenzi anaweza baada ya kukubaliana na Baraza kuwasilisha kwa Waziri mapendekezo (ambayo humu yatajulikana kama

mapendekezo ya mpango wa mafunzo) yatayo nadhimu mafunzo ya Mwanafunzi wa kazi au mwanafunzi aliyetilishwa mkataba katika kazi yoyote.

(2) Mapendekezo ya mpango wa mafunzo kuhusiana na kazi yatahusu na kufafanua -

- (a) shuruti, ikiwa ni pamoja na umri, kiwango cha elimu kinachotakiwa kwa mwanafunzi wa kazi au mwanafunzi aliyetilishwa mkataba katika kazi hiyo;
- (b) Bila ya kuathiri masharti ya kififungu cha (2) cha kifungu cha 26 cha Sheria hii muda wa mafunzo ambao hautozidi miaka saba kwa mwanafunzi wa kazi na kwa mwanafunzi aliyetilishwa mkataba utakuwa chini ya miaka minne katika kazi wanayojifunza;
- (c) Mafunzo ya vitendo ambayo yatatolewa na muajiri kwa mwanafunzi wa kazi au mwanafunzi aliyetilishwa mkataba katika mafunzo ya kazi walioajiriwa;
- (d) mafunzi ya nadharia ambayo yatatolewa na au kugharamiwa na muajiri kwa mwanafunzi wa kazi au mwanafunzi aliyetilishwa mkataba na namna mafunzo hayo yatavyotolewa au kufundishwa;
- (e) mitihani ya kupima maaarifa (ustadi) au mitihani katika kazi ambayo mara kwa mara itatakiwa kufanywa na mwanafunzi wa kazi au mwanafunzi aliyetilishwa mkataba;
- (f) masaa ya kazi ya kawaida katika wiki au siku yoyote ambayo mwanafunzi wa kazi au mwanafunzi aliyetilishwa mkataba atatakiwa au ataruhusika kufanya kazi, pamoja na siku yoyote kabla au baada katika kipindi ambacho hupata kuwepo katika kazi mwanafunzi wa kazi au mwanafunzi aliyetilishwa mkataba anaweza kutakiwa au kuruhusiwa kufanya kazi;

- (g) muda wa mwisho baada ya saa za kazi au mwanafunzi aliyetilishwa mkataba atatakiwa au kuruhusiwa kufanya kazi katika siku ye yote au katika kipindi chochote kilichoainishwa;
- (h) kiwango cha siku za mapumziko katika kazi atazoruhusiwa mwanafunzi aliyetilishwa mkataba katika mwaka wowote wa masomo yao;
- (i) malipo kuhusiana na kipindi ambacho mwanafunzi wa kazi au mwanafunzi aliyetilishwa mkataba kutokana na sababu za mafunzo hatoweza kutoa huduma kwa mwajiri wake katika masaa ya kawaida ya kazi;
- (j) mambo yoyote ambayo Mkurugenzi baada ya kushauriana na Baraza ataona ni muhimu katika utekelezaji bora wa mpango wa mafunzo.
- (3) Mapendekezo ya mpango wa mafunzo yanaweza kuweka masharti ya mafunzo ambayo yataelezea au kutumika kwa jumla au hali maalum kuhusiana na mwanafunzi wa kazi au mwanafunzi aliyetilishwa mkataba.
- (4) Masharti tofauti yanaweza kuwekwa katika mapendekezo ya mpango wa mafunzo yatayofanywa chini ya kifungu hiki kuhusiana na makundi ya waajiri au wanafunzi wa kazi au wanafunzi waliotilishwa mkataba, pia kuweka masharti tofauti kwa kazi tofauti, katika kuweka masharti Mkurugenzi baada ya kuthibitishwa na Baraza anaweza kutumia njia zozote ambazo ataona zinafaa katika kutafautisha masharti hayo.
- (5) Kabla kuwasilishwa mapendekezo yoyote ya mpango wa mafunzo kwa Waziri, Mkurugenzi atachapisha tangazo la mapendekezo hayo katika Gazeti Rasmi la Serikali na katika Gazeti jengine ambale linapatikana Zanzibar na kuelezea pahala ambapo nakala za mapendekezo hayo zitapoweza kupatikana na katika muda usiopungua siku kumi na nne kupeleka kwa Mkurugenzi maelezo kwa maandishi kuhusiana na mapendekezo hayo. Mkurugenzi kwa kushauriana na Baraza atazingatia maelezo

Isipokuwa Mkurugenzi atapeleka kwa Waziri mapendekezo iwapo hakuna maelezo yaliyotumwa katika muda uliowekwa kuhusiana na mapendekezo ya mpango wa Mafunzo.

Uwezo wa
Waziri
kufanya
Mpango wa
Mafunzo.

24.(1) Pale ambapo Waziri atastakbadhi mpango wa Mafunzo kwa mujibu wa kifungu cha 23 cha Sheria hii na akihisia kuwa inafaa kutekeleza mapendekezo hayo na pamoja na marekebisho au bila marekebisho anaweza kwa kufuatana na masharti ya kifungu hiki kutoa amri ya kufanya mpango wa masomo.

(2) Kabla ya kufanywa mpango wa masomo chini ya kijifungu cha kwanza cha kifungu hiki, Waziri atatoa tangazo katika Gazeti Rasmi la Serikali kuonyesha nia yake ya kufanya mpango wa mafunzo na kuweka masharti ya mpango unaokusudiwa kufanywa pia kuweko muda ambao hoja kuhusiana na mpango wa mafunzo au masharti yake hoja hize zitatumwa kwa Waziri.

(3) Kila hoja itakuwa kwa maandishi na itaeleza -

(a) sababu za kutowafiki;

(b) kuondoa, nyongeza au marekebisho yanayotakiwa;

na Waziri atakiria hoja yao yote itayofanywa na kupelekwa kwa Waziri na au kwa hiaba ya mtu yeyote ambaye anahisi inamhusu katika muda ytaopangwa katika Tangazo lakini tu Waziri hatolazimika (bound) kuzingatia hoja yoyote.

(4) Baada ya kuzingatia hoja ambazo zimefikishwa kwa Waziri kuzingatiwa chini ya kifungu cha (3) cha kifungu hiki, Waziri anaweza -

(a) kuendelea kutoa tangazo la mpango uliopendekezwa na yeye pamoja na marekebisho ambayo anahisi yanafaa isipokuwa hakuna mpango ambao utaondoa au kubadilisha makubaliano ya mkataba uliofikiwa na kusajiliwa baina ya mwanafunzi wa kazi au mwanafunzi aliyetilishwa mkataba kabla ya tarehe ya kupanga mpango au;

(b) kutupilia mbali nia ya kufanya mpango uliopendekezwa na badala yake kutotoa tangazo la kufanya mpango wa masomo.

(5) Kila Tangazo la kufanya mpango wa masomo litachapishwa katika Gazeti Rasmi la Serikali na katika angalau gazeti moja ambalo linapatikana Zanzibar. Tangazo hilo litaanza kutumika tarehe ambayo litachapishwa katika Gazeti Rasmi au tarehe ambayo itaainishwa katika Tangazo hilo.

(6) Mpango unawezaukafanyiwa marekebisho na mpango mwingine au kwa tangazo ambalo litalotangazwa na Waziri baada ya ushauri wa Mkurugenzi baada ya kushauriana na Baraza.

25.(1) Kila muajiri wa mwanafunzi wa kazi au mwanafunzi aliyetilishwa mkataba atateua kwa jina mmoja kati ya waajiriwa wake.

(a) mtu atayekuwa dhamana wa usimamizi wa mafunzo ya mwanafunzi wa kazi au mwanafunzi aliyetilishwa mkataba kwa jumla kwa mujibu wa masharti ya sheria hii na mpango wowote unaohusika; na

(b) katika eneo au sehemu ya kazi ambapo mwanafunzi wa kazi au mwanafunzi aliyetilishwa mkataba watakuwa kwa kawaida wakishughulikia katika kipindi kisichopungua miezi mitatu, Mwalimu wa wanafunzi wa kazi au wanafunzi waliotilishwa mkataba atakuwa dhamana wa kuongoza shughuli za kazi au ufundi wa siku hadi siku.

(2) Mkurugenzi anaweza, kwa kutoa Tangazola maandishi kwa muajiri kukataa uteuzi wa Mwalimu wa mwanafunzi wa kazi au mwanafunzi aliyetilishwa mkataba ambaye atahisi na kumudu shughuli zake kwa madhumuni ya Sheria hii, pia kwa Tangazo hilo anaweza kuainisha aina ya mafunzo ambayo Mkurugenzi atamtaka Mwalimu wa mwanafunzi wa kazi au mwanafunzi aliyetilishwa mkataba kupata kabla ya kuteuliwa kwake hakujathibitishwa tena.

(3) Pale ambapo idadi ya wanafunzi wa kazi au wanafunzi waliotilishwa mkataba au wanafunzi wa kazi na wanafunzi waliotilishwa mkataba itakuwa ishirini na tano au zaidi katika sehemu moja ya kazi. Mwalim wa wanafunzi wa kazi au wanafunzi waliotilishwa mkataba katika sehemu hiyo atatumia muda wake wote wa kawaida wa masaa ya kazi kwa kutoa mwongozo kwa wanafunzi wa kazi au wanafunzi waliotilishwa mkataba, pale ambapo idadi ya

wanafunzi wa kazi wanafunzi waliotilishwa mkataba au kwa pamoja wanafunzi wa kazi na wanafunzi waliotilishwa mkataba itapungua ishirini na tano mwalimu wa wanafunzi wa kazi au wanafunzi waliotilishwa mkataba atatumia muda wake katika kutoa mwongozo kulingana na idadi ya wanafunzi wa kazi au wanafunzi waliotilishwa mkataba au kwa pamoja wanafunzi wa kazi na wanafunzi waliotilishwa mkataba walioajiriwa.

(4) Muajiri ye yote ambaye hatofanya uteuzi unaohitajika kufanywa chini ya kijifungu (1) cha kifungu hiki au ambaye hatohakikisha kwamba masharti ya kijifungu cha (3) cha kifungu hiki atakuwa mkosa.

SEHEMU YA TANO

UWEZO WA MKURUGENZI NA

UTEUZI NA UWEZO WA WAKAGUZI.

Uwezo wa
Mkurugenzi.

26.(1) Iwapo mwanafunzi wa kazi au mwanafunzi aliye-tilishwa mkataba hatokuwepo kazini kwa muda wa siku thalathini au zaidi au kwa vipindi ambavyo kwa pamoja vinafikia idadi ya siku thalathini au zaidi Mkurugenzi anaweza akiona inafaa, kuamuru muda wake wa mafunzo uongezwe kwa idadi ya siku ambazo hakuwepo kazini, na mkataba wako utaongezwa muda kama itavyoamriwa.

(2) Iwapo itatihabitika na kutoshelezeka kwa Baraza kwamba mtu aliwahi kupata mafunzo yanayohusika katika kazi au mafunzo katika fani anayotaka kujifunza, Baraza linaweza kuamuru Mkurugenzi kumpunguzia mtu huyo muda wa kujifunza kwa kipindi ambacho kitaamuliwa.

(3) Mkurugenzi atakuwa na uwezo wote ambao atakuwa nao Mkaguzi chini ya Sheria hii.

Uteuzi wa
Wakaguzi

27. Waziri anaweza kuteua Afisa wa kazi au mtu ye yote aliyeteuliwa katika huduma za Serikali kama Mkaguzi wa Viwanda au Afisa wa Mafunzo ya Viwandani au Mkaguzi wa kazi kuwa Mkaguzi kwa madhumuni yote au yoyote ya Sheria hii.

Uwezo wa
Mkaguzi.

28.(1) Mkaguzi ye yote anaweza -

- (a) kuingia ndani ya jengo akifuatana na Afisa wa Polisi katika wakati muafaka ambalo atakuwa na sababu maalum kuamini kwamba mwanafunzi wa kazi au mwanafunzi aliyetilishwa mkataba anaeajiriwa au ameshaaajiriwa katika kipindi cha miezi sita iliyopita;
 - (b) kukagua mambo yanayohusiana na Sheria hii, iwapo atamuona mtu ye yote katika jengo ambaye ameingizwa chini ya aya (a) ya kifungu hiki au ambaye atakuwa na sababu maalum ambazo zitamfanya kuamini kwamba huyo amejiriwa au ameshaaajiriwa katika sehemu hiyo katika kipindi cha miezi sita iliyopita. Pia anaweza kumtaka mtu huyo kuchunguzwa;
 - (c) kumtaka mwanafunzi wa kazi au mwanafunzi aliyetilishwa mkataba kufika mbele yake wakati na pahala ambapo patapangwa na mkaguzi kwa madhumuni ya kumsaili mwanafunzi wakazi au mwanafunzi aliyetilishwa mkataba;
 - (d) kutaka kumbukumbu na hati zote zilizowekwa chini ya sheria hii au kanuni zilizofanywa chini ya Sheria hiikutolewa au kuwasilishwa, na shughuli zozote ambazo Mkaguzi atakuwa na sababu maalum za kuamini mtu huyo ni au alikuwa muajiri wa mwanafunzi wa kazi au mwanafunzi aliyetilishwa mkataba katika kipindi cha miezi sita iliyopita.
 - (e) kuangalia na kutoa nakala kutokana na zilizotolewa au kuwasilishwa.
- (2) Mtu yeyote ambaye -
- (a) atakataa au kutotii kwa uwezo wake wote matakwa ya Mkaguzi chini ya kifungu hiki, au
 - (b) atamzuia Mkaguzi katika kutekeleza kazi zake chini ya kifungu hiki, atakuwa mkosa.

Isipokuwa mtu ye yote hatotakiwa chini ya kifungu hiki kujibu maswali yoyote ambayo au kutoa maelezo yoyote ambayo yataamletea kujitia hatiani.

(3) Mkaguzi yeyote anayetokeleza au anayetaka kutekeleza uwezo aliopewa chini ya kifungu (1) cha kifungu hiki atatakiwa kutoa ushahidi wa maandishi wa uteuzi wake.

SEHEMU YA SITA

KUFUTWA KWA SHERIA NA VIFUNGU VYA

MCHANGANYIKO

Kutoa
maelezo
ni kosa.

29. Mjumbe yeyote wa Baraza au Afisa wa Serikali ambaye atatoa kwa mtu ye yote, isipokuwa kwa madhumuni ya kutekeleza kazi zake kwa kutekeleza uwezo aliopewa chini ya Sheria hii maelezo yoyote yanayohusiana na mambo ya fedha au kiwanda au kifaa cha mtu ye yote, maelezo hayo yakiwa yamepatikana katika utekelezaji wa kazi zake au katika kutekeleza uwezo aliopewa chini ya Sheria hii, atakuwa ninkosa.

Isipokuwa kifungu hiki hakitohusu maelezo ambayo yatatolewa kwa madhumuni ya uendesaji wa mashitaka ya jinai ambayo yatatolewa kuhusiana na Sheria hii au vyenginevyo au kwa madhumuni ya ripoti ya uendesaji wa mashitaka hayo.

Kanuni.

30.(1) Waziri anaweza kuweka Kanuni kwa ajili ya utekelezaji wa masharti na madhumuni ya Sheria hii na bila ya kuathiri uwezo wa jumla wa kufanya Kanuni, anaweza kufanya Kanuni kufafanua -

- (a) muda kushika ofisi kwa Wajumbe wa Baraza, "Quorum" pamoja na taratibu za mikutano ya Baraza namambo mengine ambayo Waziri ataona yanafaa kufafanuliwa au kuhusu Baraza pamoja na Wajumbe wake;
- (b) sampuli ya mkataba wowote wa uanafunzi wa kazi au wa kuandikishwa mkataba na mambo ambayo masharti yatawekwa kwenye mkataba huo.
- (c) taratibu ambazo viwango vya elimu au uzawa (birth) utavyoweza kuthibitishwa;
- (d) namna ya uwasilishaji wa maelezo ambayo mwajiri atatakiwa mara kwa mara kuwasilishwa;

- (e) taratibu kusajili na uhamishaji wa mikataba ya uanafunzi wa kazi na uanafunzi wa kutilishwa mkataba na kwa ajili ya kutoa taarifa ya kumaliza muda au kuvunjwa kwa mikataba hiyo ;
- (f) aina na taratibu ambazo zitatumika katika kutoa vyeti vya uanafunzi wa kazi na uanafunzi wa kutilishwa mkataba ambavyo vitatolewa na waajiri;
- (g) taratibu za kukata rufaa kwa Waziri chini ya Sheria hii;
- (h) mambo yote au jambo lolote ambalo Sheria hii inataka lifafamuliwe au inaruhusu kufafamuliwa.

(2) Kanuni tofauti zinaweza kuwekwa chini ya kijifungu (1) cha kifungu hiki kwa makundi tofauti ya waajiri au wanafunzi wa kazi au wanafunzi wa kutilishwa mkataba na kwa fani na kazi tofauti. Katika kufanya hivyo Waziri atatumia njia tofauti ambazo atahisi ni za busara.

Kufungua
Mashtaka.

31. Mkaguzi ye yote anaweza kufungua mashtaka kuhusiana na kosa lolote chini ya Sheria hii au Kanuni zozote zilizowekwa chini ya Sheria hii pia anaweza kuendesha mashtaka katika kesi hiyo.

Adabu.


32. Mtu ye yote ambae anafanya kosa chini ya Sheria hii na adabu yake kosa hilo haikuainishwa, iwapo kosa litathibiti atalipa faini isiyozidi shilingi elfu kumi au kifungo kwa muda usiozidi miaka mitatu au kifungo pamoja na faini.

Kufutwa kwa
Cap. 57

33.(1) Sheria ya "Apprentices" inafutwa.

(2) Bila ya kujali kufutwa kwa Sheria ya "Apprentices" na kifungu (1) cha Sheria, mkataba kila mkataba ambao ulikuwepo mara kabla ya kuanza kutumika Sheria hii utaendelea kutumika na kuandikwa, kutekelezwa na kusajiliwa kwa mujibu wa taratibu zilizowekwa katika kifungu cha 13 cha Sheria hii katika muda wa miezi minne kuanzia tarehe ya kuanza kutumika kwa Sheria hii.

Imepitishwa Na Baraza la Wawakilishi tarehe
1986.


SALIM MZEE
KAIMU KATIBU WA
BARAZA LA WAWAKILISHI
ZANZIBAR.